MUUNDO WA UTUMISHI WA UMMA WA MWAKA 2002

WACHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPUTA-COMPUTER SYSTEMS ANALYST

MCHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA DARAJA LA II-TGS.D

SIFA ZA KUAJILIWA

- KUAJIRIWA WENYE SHAHADA/STASHAHADA YA JUU KATIKA MASOMO YA SAYANSI YA KOMYUTA KUTOKA CHUO/TAASISI INAYOTAMBULIWA NA SERIKALI

KAZI ZA KUFANYA

- KUWEKA KUMBUKUMBU ZA TARATIBU ZA KISASA NA MBINU ZA KUFANYIA KAZI
- KUTEKELEZA CHATI ZA MTIRIRIKO WA MIFUMO YA NYENDO ZA TAARIFA NA UDHIBITI UNAOHUSU KOMPYUTA
- KUTOA MSAADA WA KIUFUNDI KWA WATUMISHI WA TAASISI HUSIKA ILI KUWEZESHA KUFANYA KAZI ZAO ZA KILA SIKU

MCHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA DARAJA LA II-TGS.E

SIFA ZA KUAJILIWA

- KUAJIRIWA WENYE SHAHADA/STASHAHADA YA JUU KATIKA MASOMO YA SAYANSI YA KOMYUTA KUTOKA CHUO/TAASISI INAYOTAMBULIWA NA SERIKALI NA AMBAO WANA UZOEFU WA KAZI KWA MUDA USIOPUNGUA MIAKA 5 KATIKA FANI HIYO

SIFA ZA KUINGILIA WALIOMO KAZINI

- KUPANDISHWA CHEO WACHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA DARAJA II AMBAO WAMEKUWA NA UTENDAJI MZURI WA KAZI KULINGANA NA SERA YA MENEJIMENTI NA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

KAZI ZA KUFANYA

- KUKUSANYA DATA KWA AJILI YA UCHAMBUZI WA MAENEO YA MATATIZO
- UCHAMBUZI WA KUMBUKUMBU,HATI,MAJALADA NA TAARIFA KUHUSIANA NA MTIRIRIKO WA KAZI

- KUFANYA UCHAMBUZI WA KINA WA MIFUMO YA KOMPUTA
- KUTAYARISHA HATI ZA UCHAMBUZI WA MIFUMO NA KUIFANYIA MAJARIBIO
- KUANDIKA MIONGOZO KWA WATUMIAJI WA MIFUMO KOMPYUTA
- KUSIMAMIA KITUO CHA DATA NA MTANDAO
- KUFUATILIA MFUMO WA USALAMA WA KOMPYUTA
- KUTOA MSAADA WA KIUFUNDI KWA WATUMIAJI WA KOMPYUTA

MCHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA WAANDAMIZI-TGS.F

SIFA ZA KUAJILIWA

- KUAJIRIWA WENYE SHAHADA/STASHAHADA YA JUU KATIKA MASOMO YA SAYANSI YA KOMYUTA KUTOKA CHUO/TAASISI INAYOTAMBULIWA NA SERIKALI NA AMBAO WANA UZOEFU WA KAZI KWA MUDA USIOPUNGUA MIAKA 7 KATIKA FANI HIYO

SIFA ZA KUINGILIA WALIOMO KAZINI

- KUPANDISHWA CHEO WACHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA DARAJA I AMBAO WAMEKUWA NA UTENDAJI MZURI WA KAZI KULINGANA NA SERA YA MENEJIMENTI NA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

KAZI ZA KUFANYA

- KUSHIRIKI KATIKA UCHAMBUZI WA MIFUMO YA WAKATI HALISI ILIYOSAMBAZWA YA KINA
- KUTAYARISHA HATI ZA UCHAMBUZI WA MIFUMO YA WAKATI HALISI ILIYOSAMBAZWA YA KINA
- KURATIBU UTEKELEZAJI NA KUWEPO KWA UCHAMBUZI WA MIFUMO YA WAKATI HALISI ILIYOSAMBAZWA
- KUFANYA UCHAMBUZI WA UFANISI WA MIFUMO WA MTANDAO WA KOMPYUTA ,KUTAYARISHA TAARIFA ZA UTUMIAJI NA UFANISI NA KUPENDEKEZA UBADILISHAJI NA UBORESHAJI WA VIFAA,MITAMBO NA PROGRAM ZA KOMPYUTA
- KURATIBU MAJARIBIO YA MIFUMO YA KOMPUTA
- KUTUNZA KIONGOZI CHA TARATIBU ZA HUDUMA YA KOMPYUTA KUHUSIANA NA MZUNGUKO WA UHAI WA MAENDELEO YA MFUMO
- KUHAKIKISHA UFUNGAJI SAHIHI WA MIFUMO NA MITANDAO YOTE
- KUSIMAMIA WAFANYA KAZI WALIOKO CHINI YAKO

- KUTOA MSAADA WA KIUFUNDI KWA WATUMIAJI WA KOMPYUTA
- KUBUNI MAJALADA YA DATA NA HABARI ZITOKAZO KWENYE KOMPYUTA NA MUUNDO WA TAARIFA
- KUFANYA MAREKEBISHO YA VIGEZO VYA MFUMO KILA INAPOBIDI ILI KUBORESHA UFANISI
- KUFANYA MATENGENEZO YA KILA JUMA YA KITUO CHA DATA NA KUHIFADHI DATA
- KUFUNGA NA KUPANGA UPYA VIHIFADHI DATA KWA MATUMIZI BORA ZAIDI
- KUTAFUTA MBINNU ZA KUOKOA DATA KUTOKEAPO HITILAFU
- KURATIBU KAZI ZA WACHAMBUZI W A KOMPYUTA YA KOMPUYTA DARAJA LA I

MCHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA MKUU DARAJA LA III-TGS.G

SIFA ZA KUAJILIWA

- KUAJIRIWA WENYE SHAHADA/STASHAHADA YA UZAMILI KATIKA FANI YA SAYANSI YA KOMYUTA KUTOKA CHUO/TAASISI INAYOTAMBULIWA NA SERIKALI NA AMBAO WANA UZOEFU WA KAZI KWA MUDA USIOPUNGUA MIAKA 10 KATIKA FANI HIYO

SIFA ZA KUINGILIA WALIOMO KAZINI

- KUPANDISHWA CHEO WACHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA WAANDAMIZII AMBAO WAMEKUWA NA UTENDAJI MZURI WA KAZI KULINGANA NA SERA YA MENEJIMENTI NA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

KAZI ZA KUFANYA

- KUTAYARISHA MBINU Y A UTEKELEZAJI WA MAENDELEZO
- KURATIBU SHUGHULI ZOTE ZA MZUNGUKO WA UHAI WA MAENDELEO YA UTUMIZI WA KOMPYUTA
- KUTATHMINI MIFUMO YA UTUMIZI WA VIFAA NA MITAMBO NA MAENDELEO YA PROGRAMM ZA KOMPYUTA
- KUHAKIKISHA KWAMBA UHIFADHI WA MARA KWA MARA UNAFANYWA KWA AJILI YA VIHIFADHI VYA LAN/WAN KWA MUJIBU WA TARATIBU ZILIZOAINISHWA
- KUWEKA MPANGO WA KUOKOA MAAFA YA SASA

- KUFUATILIA NA KUSIMAMIA SHHUGHULI ZOTE ZA MATENGENEZO YA VIFAA NA MITAMBO YA KOMPYUTA

MCHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA MKUU DARAJA LA II-TGS.H

SIFA ZA KUAJILIWA

- KUAJIRIWA WENYE SHAHADA/STASHAHADA YA UZAMILI KATIKA FANI YA SAYANSI YA KOMYUTA KUTOKA CHUO/TAASISI INAYOTAMBULIWA NA SERIKALI NA AMBAO WANA UZOEFU WA KAZI KWA MUDA USIOPUNGUA MIAKA 12 KATIKA FANI HIYO

SIFA ZA KUINGILIA WALIOMO KAZINI

- KUPANDISHWA CHEO WACHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA WAKUU DARAJA LA III WENYE SHAHADA/STASHSHADA YA UZAMILI KATIKA FANI YA KOMPYUTA KUTOKA TAASISI AU CHUO KINACHOTAMBULIKANA NA SERIKALI AMBAO WAMEKUWA NA UTENDAJI MZURI WA KAZI KULINGANA NA SERA YA MENEJIMENTI NA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

KAZI ZA KUFANYA

- KUPANGA, KUSIMAMIA NA KUDHIBITI KAZI ZA PROGRAMM KWA WAFANYAKAZI WA PROGRAMU NA KUMSAIDIA MKURUGENZI KATIKA KAZI ZA MIFUMO KWA KILA MFANYAKAZI.
- KUSIMAMIA MAJARIBIO YA MIFUMO KUHUSIANA NA MAENDELEO YA VIFAA NA MITAMBO MIPYA NA /AU PROGRAMU MPYA ZA KOMPYUTA VITAKAVYOSAIDIA WAFANYAKAZI WA MATUMIZI YA PROGRAMU.
- KUTOA MAPENDEKEZO KWA AJILI NA AU KUSAIDIA TATHMINIYA VIFAA NA MITAMBO MIPYA NA/AU PROGRAMU MPYA ZA KOMPYUTA VITAKAVYOSAIDIA WAFANYAKAZI WA MATUMIZI YA PROGRA.
- KUWASAIDIA WACHAMBUZI TAARIFA NA KUMBUKUMBU NA KUANDAA MAHITAJI YA AWALI YA MFUMO KUHUSIANA NA WATUMIAJI
- KUFANYA UCHAMBUZI WA KILA JUMA WA MIRADI ILIYOPO NA AMBAYO HAIJATEKELEZWA ILI KUHAKIKISHA UTOAJI WA TAARIFA ZA MENEJIMENTI KWA WAKATI ULIOPANGWA.

MCHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA MKUU DARAJA LA I-TGS.I

SIFA ZA KUAJILIWA

- KUAJIRIWA WENYE SHAHADA/STASHAHADA YA UZAMILI KATIKA FANI YA SAYANSI YA KOMYUTA KUTOKA CHUO/TAASISI INAYOTAMBULIWA NA SERIKALI NA AMBAO WANA UZOEFU WA KAZI KWA MUDA USIOPUNGUA MIAKA 15 KATIKA FANI HIYO

SIFA ZA KUINGILIA WALIOMO KAZINI

- KUPANDISHWA CHEO WACHAMBUZI WA MIFUMO YA KOMPYUTA WAKUU DARAJA LA II WENYW SHAHADA/STASHAHADA YA UZAMILI KATIKA FANI YA KOMPYUTA KUTOKA KATIKA CHUO/TAASISI INAYOTAMBULIWA NA SERIKALI NA AMBAO WAMEKUWA NA UTENDAJI MZURI WA KAZI KULINGANA NA SERA YA MENEJIMENTI NA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

KAZI ZA KUFANYA

- KUTAYARISHA NA KUTUNZA MIONGOZO, TARATIBU NA VIWANGO VYA MIFUMO.
- KUSIMAMIA UFUNGAJI , MAJARIBIO NA MATENGENEZO YA VIHIFADHI VYOTE/PROGRAMU ZA KOMPUTA NA VIFAA NA MITAMBO VYA MAWASILIANO YA SIMU
- KUWA KAMA KIUNGO KATI YA MAENEO MENGINE YA KITUO CHA DATA NA PROGRAMMU ZA KOMPYUTA
- KUHAKIKISHA KWAMBA KUNAKUWEPO NA MSAADA WA KUTOSHA KWA WATUMIAJI WA KOMPYUTA KUHUSIANA NA MIFUMO YA MSAADA WA TAARIFA NA KUMBUKUMBU
- KUWEKA TARATIBU, SHERIA NA KANUNI ZA UTUNZAJI KUMBUKUMBU ZINAZOHITAJIKA KWA KUENDELEZEA MUUNDO MBINU NA TEKNOLOJIA YA HABARI UNAOFAA NA WENYE UFANISI.